

NI

USHINDI

Mwandishi: MAUMBBA S.B

Kwanza kabisa naomba nikupongeze wewe kwa kuweza kujipatia nakala hii ya kitabu hiki cha USHINDI. Naomba nikuambie kuwa wewe ni ushindi na ndani ya kitabu hiki tutaongelea huo Ushindi.

Hakuna mtu nayependa kushindwa duniani. Yani kila mtu hufanya jambo fulani akitamani na kutarajia Ushindi katika lile jambo analolifanya.

Mwanariadha anapozianza mbio zake huwa anatarajia Ushindi. Mchezaji wa mpira wa miguu pia timu yake inapoingia uwanjani huwa anachokitarajia ni Ushindi. Vile vile kwa wanafunzi wanapokuwa mashulen ihusoma kwa juhudi sana wakihitajia Ushindi.

Kwahiy o neno ushindi sio geni sana. Kwa sababu hata wewe unapokwenda kazini huwa unatarajia kupata Ushindi katika kazi na majukumu yako ya kila siku.

Lakini leo hii nataka nikuoneshe kuwa neno hili hili la Ushindi linaweza kutazamwa katika njia na jicho la kipekee sana.

Maana ya Ushindi iliyo kiini cha kitabu hiki, huenda ikawa tofauti kidogo na ile ya kawaida iliyo zoleka. Nataka kukujuza kuhusu U.S.H.I.N.D.I wa kweli kweli. Ushindi ambao jamii inahitaji kuupambania ili kuusimamisha.

Ni upi huo USHINDI?. Endelea kusoma chapter inayofuata.